JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA

SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA

ISO 9001:2015 Certified

*Mwanachama wa Shirika la Viwango la Kimataifa (ISO), Codex Alimentarius Commission (WHO/FAO) na Wakala wa ISO na Mashirika ya Viwango ya Mataifa mbalimbali*

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MATUMIZI YA MCHANGANYIKO WA SUKARI NA VIKOLEZA UTAMU (ARTIFICIAL SWEETENERS) KWENYE VINYWAJI LAINI VYENYE KABONI (CARDONATED SOFT DRINK)

**Dar es salaam, 26 Julai 2022**

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) limepewa jukumu la kusimamia usalama na ubora wa bidhaa za chakula kupitia Viwango Sura ya 130. Shirika linatekeleza jukumu hili kupitia kanuni ya usajili na udhibiti wa shehena ya mwaka 2021.

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) limekuwa likitoa elimu mara kwa mara kuhusiana na ubora na usalama wa bidhaa za chakula zinazozalishwa nchini na zinazoingia kutoka nje ya nchi ikiwa ni juhudi za Shirika kuhakikisha usalama wa chakula kinachotumika nchini.

Licha ya elimu kubwa inayotolewa juu ya taratibu bora za uzalishaji, uhifadhi na usambazaji wa bidhaa za chakula, Shirika limebaini kuwepo kwa baadhi ya wafanyabiashara ambao bado wanakiuka taratibu zilizowekwa hasa kwenye vinywaji laini (carbonated soft drinks) kwa kuingiza bidhaa zenye mchanganyiko wa sukari na vikoleza utamu (artificial sweeteners) kinyume na matakwa ya viwango vilivyowekwa.

Kwa kawaida vinywaji vyenye vikolezo utamu huzalishwa kwa ajili ya mahitaji ya kundi fulani la wateja kwa mfano wenye matatizo ya kisukari au wanaotaka kupunguza uzito n.k. kwa kuwa vikoleza utamu hivyo havina sukari (yaani *sucrose*).

Kwa mujibu wa kiwango cha kitaifa cha vinywaji laini vyenye kaboni (*TZS 390:2019 (E) – Carbonated Soft drinks)* kinakataza kuchanganya sukari na vikoleza utamu (*Artificial sweeteners*).

Hivyo bidhaa za vinywaji laini vyenye kaboni ambavyo havina sukari (*sugar free*) vimeruhusiwa kutengenezwa kwa kutumia vikoleza utamu pekee (*100% artificial sweeteners*) bila kuchanganya na sukari kwa mujibu wa kiwango cha kitaifa (*TZS 2330:2019 (E): Sugar free carbonated soft drinks – specification*).

Aidha kwa bidhaa zenye vikoleza utamu pekee (*100% artificial sweeteners*), kwa mujibu wa kiwango cha bidhaa hizo, mzalishaji anatakiwa kuainisha uwepo wa vikoleza utamu hivyo na kuweka tahadhari ya kutotumika kwa makundi maalumu ya watu kama vile watoto, wamama wenye ujauzito na wanao nyonyesha.

Shirika linapenda kuwakumbusha waingizaji wote wa bidhaa za vyakula hasa wale wenye maduka makubwa (*supermarke*t) ambao wana utaratibu maalumu wa kusajili bidhaa zao, kuzingatia matakwa ya viwango na kuingiza bidhaa za vinywaji laini (Carbonated soft drinks) ambazo hazina mchanganyiko wa sukari na vikoleza utamu (artificial sweeteners).

Ili kulinda afya za watumiaji na makundi maalum kama yalivyotajwa hapo juu, TBS itafuatilia kwa ukaribu bidhaa hizo na hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa wote wanaokiuka taratibu zilizowekwa.

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) litaendelea kuhakikisha kuwa matakwa ya Sheria kuhusiana na ubora na usalama wa bidhaa za chakula unazingatiwa na wadau wote ili kuepuka athari za kiafya zinazoweza kujitokeza.

Kwa taarifa zaidi wasiliana na: -

**Mkurugenzi Mkuu,**
Shirika la Viwango Tanzania (TBS),
SLP 9524,
Dar es Salaam.
Simu: +255(022)2450298/Hotline: 0800110827
Barua pepe: info@tbs.go.tz/ Tovuti: www.tbs.go.tz/ malalamiko@tbs.go.tz

**TBS MAKAO MAKUU**
Shirika la Viwango Tanzania
Barabara ya Sam Nujoma /
Morogoro, Ubungo, Dar es Salaam
S. L. P. 9524
DAR ES SALAAM, TANZANIA
Simu Na: +255 22 245 0298/
+255 22 245 0206
Nukushi: +255 22 2450959
Namba ya Simu Bila Malipo: 0800110827
Barua pepe: info@tbs.go.tz
Tovuti: http://www.tbs.go.tz
Barua pepe kwa ajili ya malalamiko ya wateja: malalamiko@tbs.go.tz
Twitter: TBS_Tanzania
Instagram: tbs_Viwango

**TBS KANDA YA KATI**
Jengo la Kambarage
S. L. P. 2956
DODOMA,
TANZANIA
Simu Na:
+255 26 2520310

**TBS KANDA YA ZIWA**
Jengo la NSSF,
Ghorofa ya 3
S. L. P. 1814
MWANZA,
TANZANIA
Simu Na:
+255 28 2505044

**TBS KANDA YA KASKAZINI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 2399
ARUSHA,
TANZANIA
Simu Na:
+255 27 2520143

**TBS KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI**
Jengo la NHIF,
Ghorofa ya 7
S. L. P. 1674
MBEYA, TANZANIA
Simu Na:
+255 25 2502848

**TBS KANDA YA KUSINI**
Jengo la MTUWASA
S. L. P. 1396
MTWARA,
TANZANIA
Simu Na:
+255 23 2334477

**TBS KANDA YA MAGHARIBI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 1276
KIGOMA,
TANZANIA
Simu Na:
+255 28 2804023

Barua zote ziandikwe kwa **MKURUGENZI MKUU**